# TPDC

JARIDA LA JUNI, 2025

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA

TOLEO LA 26 www.tpdc.co.tz tpdc.tz




## TPDC YATOA GAWIO LA SHILINGI BILIONI 11.7 KWA SERIKALI

Uk. 4



## YALIYOMO


- LESOTHO YAJIFUNZA KUHUSU SEKTA YA NISHATI
- TPDC YATOA GAWIO LA SHILINGI BILIONI 11.7 KWA SERIKALI
- TPDC YAENDESHA BONANZA KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI MTWARA
- MAKAMANDA WA JESHI LA POLISI WATEMBELEA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA
- NAIBU KATIBU MKUU ZUHURA YUNUS AIPONGEZA KAMPUNI TANZU YA GASCO
- DC LINDI AIPONGEZA TPDC, SHELL NA EQUINOR KUWEZESHA VIJANA MAFUNZO YA VETA LINDI
- UZINDUZI WA MPANGO MKAKATI WA TPDC WA MIAKA 25 JIJINI DODOMA
- MKUU WA MKOA WA SINGIDA, MHE. HALIMA DENDEGO, ATEMBELEA BANDA LA GASCO KATIKA MAONESHO YA WIKI YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI
- MKUTANO WA TEKNOLOJIA BARANI AFRIKA
- TPDC YAKABIDHI VIFAA VYA OFISI KWA JESHI LA POLISI MTWARA
- TPDC YATOA ELIMU KWA JAMII ZA WAVUVI KUHUSU MRADI WA UTAFUTAJI MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA KITALU CHA EYASI WEMBERE
- TPDC YADHAMINI NA KUSHIRIKI MBIO ZA MARATHONI KWA LENGO LA KUELIMISHA UMMA MATUMIZI YA NISHATI SAFI
- TPDC YATUNUKIWA TUZO YA UHIFADHI MAZINGIRA
- MHE. KAPINGA AZINDUA KITUO MAMA CHA KUSHINDILIA GESI ASILIA KWENYE MAGARI
- HABARI KATIKA PICHA



# LESOTHO YAJIFUNZA KUHUSU SEKTA YA NISHATI

**Dar es salaam,**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Nchini Lesotho, Bw. Tonkiso Phapano, aliongoza ujumbe maalum kuja Tanzania kwa ziara ya kimafunzo iliyoangazia namna bora ya kusimamia na kuendeleza sekta ya nishati, hasa kwenye sekta ndogo za mafuta na gesi asilia.


Katika ziara hiyo, ujumbe wa Lesotho ulipata fursa ya kutembelea Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kupata maelezo ya kina kuhusu shughuli zinazotekelezwa nchini katika muktadha wa nishati ya mafuta na gesi.

"Tumevutiwa sana na jinsi Tanzania inavyosimamia sekta ya nishati. Tulivutiwa zaidi na wasilisho lenu wakati wa Mkutano wa Nishati wa Mission 300. Tupo kwenye mchakato wa maboresho ya sheria zetu za nishati na hatukuona mfano bora zaidi ya Tanzania," alisema Phapano.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa TPDC, Bw. Derick Moshi, akimuwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika, aliukaribisha ujumbe huo na kusisitiza kuwa TPDC iko tayari kushirikiana kwa karibu na nchi rafiki katika kubadilishana maarifa na uzoefu.

"TPDC ilianzishwa mwaka 1969 na kuanza rasmi shughuli zake mwaka 1973. Tunatekeleza majukumu yetu kupitia idara mbalimbali pamoja na kampuni tanzu mbili ambazo ni GASCO, inayosimamia mitambo ya gesi asilia, na TANOIL, inayojihusisha na biashara ya mafuta," alisema Moshi.

Aidha, alieleza kuwa Tanzania imegundua kiasi kikubwa cha gesi asilia, ambacho huzalishwa na kutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya kupikia majumbani, viwandani, kwenye magari na kuzalisha umeme.




**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TPDC Mhe. Ombeni Sefue akikabidhi Hundi ya Gawio la Serikali kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Ikulu, Jijini Dar es salaam**

# TPDC YATOA GAWIO LA SHILINGI BILIONI 11.7 KWA SERIKALI

**Dar es salaam,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilitoa gawio la shilingi Bilioni 11.7 kwa Serikali kwa mwaka 2025, likiwa ni ongezeko mara mbili walilotoa mwaka jana 2024 shilingi Bilioni 5.8.

Gawio hilo lilitolewa tarehe 10.06. 2025 Ikulu Jijini Dar es Salaam na kupokelewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika hafla ya kupokea gawio na michango kutoka kwa taasisi na mashirika ya umma.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali na taasisi husika, wakiwemo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TPDC Mhe. Balozi Ombeni Sefue pamoja na Mkurugenzi Mtendaji TPDC, CPA Mussa Makame.

Aidha, Rais Samia alipokea jumla ya shilingi trilioni 1.028 ikiwa ni gawio na michango kutoka kwa mashirika ya umma yaliyo chini ya usimamimizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina (OMH) na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.



# TPDC YAENDESHA BONANZA KWA WANAFUNZI WA SEKONDARI MTWARA

**Mtwara,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) liliendesha bonanza kwa Wanafunzi kutoka baadhi ya shule za Sekondari mkoani Mtwara kwa lengo la kuendeleza uhusiano na ujirani mwema katika Shule hizo.

Akizungumza wakati wa bonanza hilo la Wanafunzi mkoani humo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo la TPDC, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Bi. Marie Msellemu alisema TPDC inazidi kuendeleza uhusiano na ujirani mwema mashuleni ikiwa ni pamoja na kuanzisha klabu za TPDC zinazotoa elimu juu ya namna nzuri ya matumizi ya gesi asilia.

Aidha, bonanza hilo lilifanyika katika Shule ya Sekondari ya Mangamba iliyopo Manispaa ya Mtwara Mikindani ikijumuisha michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa pete, kukimbia kwenye gunia pamoja na kufukuza kuku.

"TPDC inazidi kuendeleza uhusiano na ujirani mwema mashuleni ikiwa ni pamoja na kuanzisha klabu za TPDC zinazotoa elimu juu ya namna nzuri ya matumizi ya gesi asilia," alisema Msellemu.

Vilevile, Msellemu aliwaomba Wanafunzi wa Sekondari za Msimbati, Naliendele, Mangamba na Ziwani mkoani Mtwara kuwa mabalozi wazuri na walinzi wa miundombinu ya gesi asilia katika maeneo yanayowazunguka.

Bonanza hilo limetamatika kwa Shule ya Sekondari ya ziwani kutwaa ubingwa katika mchezo wa mpira wa miguu kwa mikwaju minne ya penati dhidi ya wapinzani wake mangamba sekondari wakipoteza kwa penati tatu. Baadhi ya wanafunzi walioshiriki bonanza hilo waliishukuru TPDC kwa kuandaa mashindano hayo kwani kupitia michezo kama hiyo husaidia kuibua vipaji mbalimbali kwa vijana.

Waliongeza kuwa bonanza hilo limesaidia kuimarisha uhusiano mzuri baina ya shule moja na nyingine katika sekta ya michezo na taaluma hivyo waliiomba TPDC kuendeleza kuratibu michezo hiyo.

Shule zilizoshiriki bonanza hilo ni Sekondari za Msimbati, Naliendele, Mangamba na Ziwani.



# MAKAMANDA WA JESHI LA POLISI WATEMBELEA MIUNDOMBINU YA GESI ASILIA

**Mtwara,**

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi Tanzania, CP Awadhi Juma Haji, aliongoza Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara ambayo ni mikoa inayopitiwa na miundombinu ya gesi asilia na kufanya ziara ya ukaguzi wa miundombinu hiyo inayotoka Msimbati, Madimba hadi Kinyerezi kupitia Somanga.

Ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na Kampuni ya GASCO inayosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Akizungumza wakati wa ukaguzi huo, CP Awadhi alibainisha kuwa Jeshi la Polisi lina wajibu wa kuhakikisha miundombinu ya gesi asilia inakuwa katika hali ya usalama wa kutosha, kwa kuwa rasilimali hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

"Jeshi la Polisi lina makubaliano ya ushirikiano na Kampuni ya GASCO kupitia TPDC kwa ajili ya kutoa ulinzi kwenye miundombinu ya gesi asilia. Ziara hii ni utekelezaji wa takwa la makubaliano hayo, ambapo kila mwaka tunatakiwa kufanya ukaguzi ili kutathmini hali ya kiusalama," alisema CP Awadhi.

CP Awadhi alisema, ukaguzi huo unaangazia tathmini ya hali ya usalama katika kipindi kilichopita, kutambua changamoto zilizojitokeza na namna zilivyoshughulikiwa, pamoja na kupanga mikakati



**Makamanda wa Jeshi la Polisi wa Mikoa ya Dar es salaam, Pwani,Lindi na Mtwara wakiwa katika ziara ya kutembelea miundombinu ya gesi asilia iliyopo Madimba, mkoani Mtwara**

ya kuimarisha zaidi ulinzi wa miundombinu hiyo.

"Nichukue fursa hii kuwashukuru wenzetu wa GASCO na TPDC kwa ushirikiano mkubwa walioutoa katika kuandaa ziara hii. Ushirikiano huu unatupa nafasi ya kufanya tathmini ya pamoja ya hali ya kiusalama kwenye maeneo yote ya miundombinu ya gesi asilia," ameongeza.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Usalama GASCO, Bw. Fred Mfikwa alieleza kuwa mbali na vyombo vya dola, GASCO pia imeingia mikataba na Vijiji vinavyopitiwa na miundombinu hiyo, ambapo Wananchi hushiriki katika shughuli za ulinzi na usafi wa maeneo yanayopitiwa na miundombinu ya gesi asilia.

Mfikwa alisema hatua hii imeongeza urafiki kati ya TPDC na jamii, hali inayowasaidia kupokea taarifa muhimu za kiusalama na kutambua mapema hitilafu zinazoweza kutokea. Aidha, ametoa pongezi kwa Jeshi la Polisi kwa namna lilivyo mstari wa mbele katika kushughulikia changamoto za kiusalama.

"Kwa kipindi chote tangu tuingie makubaliano na Jeshi la Polisi, hatujakumbwa na changamoto yoyote kubwa. Polisi wamekuwa wakijitokeza haraka tunapohitaji msaada, na hatua za kisheria huchukuliwa kwa wanaoharibu au kuingilia miundombinu yetu," alisema Mfikwa.

# NAIBU KATIBU MKUU ZUHURA YUNUS AIPONGEZA KAMPUNI TANZU YA GASCO




**Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Bi. Zuhura Yunus akipewa maelezo ya namna GASCO inavyozingatia usalama wa wafanyakazi mahala pa kazi na Afisa Usalama na Mazingira Mahala Pa Kazi wa Kampuni Tanzu ya GASCO Bi. Suzana Masaba**

**Singida,**

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Bi. Zuhura Yunus alitembelea banda la Kampuni ya GASCO ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika maonesho ya Wiki ya Usalama Mahala pa Kazi yaliyofanyika Mkoani Singida.

Katika ziara hiyo, Bi. Zuhura Yunus alipata fursa ya kujionea jitihada mbalimbali zinazofanywa na GASCO katika kuhakikisha mazingira salama na yenye afya kwa wafanyakazi wake, sambamba na kuzingatia viwango vya usalama katika shughuli za uendeshaji na matenegezo ya mitambo ya Uchakataji, Usafirishaji na Usambazaji Gesi Asilia hapa nchini

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Bi. Zuhura aliipongeza GASCO kwa kuonesha dhamira na juhudi madhubuti katika kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wake, na kusisitiza umuhimu wa kuendeleza juhudi hizo ili

kulinda rasilimali watu na kuimarisha tija mahala pa kazi.

"Naipongeza GASCO kwa kujidhihirisha kama taasisi yenye dhamira ya kweli na juhudi za hali ya juu katika kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wake. Hatua hizi si tu zinajenga mazingira bora ya kazi bali pia zinaakisi uelewa wa kina kuhusu umuhimu wa rasilimali watu katika maendeleo endelevu ya taasisi. Ni rai yangu kwamba juhudi hizi ziendelezwe na kuimarishwa zaidi, ili kuendelea kuhamasisha ustawi wa wafanyakazi na kuleta tija inayokusudiwa katika maeneo ya kazi,"alisema Zuhura.

Maonesho haya yamelenga kuhamasisha taasisi na mashirika yote nchini kuhusu umuhimu wa kuzingatia viwango vya usalama na afya kazini kwa ustawi wa wafanyakazi na maendeleo ya taifa kwa ujumla.




**Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Bi. Zuhura Yunus akikabidhiwa zawadi na Watumishi wa Kampuni Tanzu ya GASCO alipotembelea banda la GASCO wakati wa maonesho ya Wiki ya Usalama Mahala Pa Kazi mkoani Singida**

# DC LINDI AIPONGEZA TPDC, SHELL NA EQUINOR KUWEZESHA VIJANA MAFUNZO YA VETA LINDI

**Lindi,**

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Mhe. Victoria Mwanziva, alitoa pongezi kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Kampuni za kimataifa za nishati Shell na Equinor kwa kuratibu na kufadhili programu ya mafunzo ya ufundi stadi kupitia VETA. Mafunzo hayo yamwanufaisha vijana 24 wa Wilaya ya Lindi.

Mhe. Mwanziva alikuwa Mgeni Rasmi katika Mahafali ya ngazi ya 3 ya VETA kwa vijana hao, ambapo alisisitiza umuhimu wa mafunzo hayo katika kuwawezesha vijana kujiajiri na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi ya Lindi. “Mafunzo haya ya ufundi stadi ni uwekezaji muhimu katika siku zijazo za vijana wetu. Yanawapa ujuzi unaohitajika kujitegemea na kuunda fursa zao wenyewe,” alisema Mhe. Mwanziva.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Bw. Ally Mluge, Afisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi, alieleza kuwa TPDC imekuwa ikishirikiana kwa karibu na kampuni za kimataifa za nishati kuratibu utekelezaji wa miradi ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) kulingana na Sheria ya Mafuta ya mwaka 2025. Ushirikiano huo unahakikisha kwamba faida za rasilimali za nishati zinanufaisha jamii moja kwa moja.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Kampuni ya Shell, Dkt. Naomi Makota, alitoa maelezo juu ya umuhimu wa programu hiyo katika kukuza ushirikiano imara kati ya kampuni hizo na jamii. Alisisitiza kuwa programu hizo ni muhimu kwa kujenga uhusiano wa kudumu na kuleta maendeleo endelevu.

Mpango huu wa mafunzo ya VETA, unaofadhiliwa kwa pamoja na Kampuni ya Shell na Equinor, unawakilisha mfano mzuri wa jinsi ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi unavyoweza kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya vijana na kukuza maendeleo ya jamii. Vijana hawa 24 wamepewa vifaa vya kisasa na sasa wako tayari kuanza safari yao ya ujasiriamali na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Wilaya ya Lindi.



**Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mhe. Victoria Mwanziva, akitoa hotuba mbele ya wahitimu wa mafunzo ya ngazi ya tatu (hawapo pichani) katika mahafali ya VETA-Lindi, mafunzo ambayo yanafadhiliwa na Makampuni wabia wa mradi wa LNG, Shell na Equinor**



**Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mhe. Victoria Mwanziva, akiwa katika picha ya pamoja na moja ya wanafunzi (wa tatu kutoka kulia) waliohitimu mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya tatu na kupewa cherehani (kifaa cha kazi). Wengine pichani ni wawakilishi wa Kampuni na Taasisi mbalimbali ikiwemo PURA, TPDC, Shell, Equinor na VETA-Lindi**



**Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mhe. Victoria Mwanziva, pamoja na wageni kutoka PURA, TPDC, Shell na Equinor wakiwa katika picha ya pamoja na Wahitimu wa ngazi ya tatu ya ufundi stadi katika mahafari yaliyofanyika katika viwanja vya chou cha VETA-Lindi**

# UZINDUZI WA MPANGO MKAKATI WA TPDC WA MIAKA 25 JIJINI DODOMA



**Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Doto Biteko (katikati) akiwa na Viongozi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa TPDC wa miaka 25 Jijini Dodoma**

**Dodoma,**

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, alilielekeza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuongeza kasi ya uendelezaji wa vitalu vya utafutaji wa mafuta na gesi asilia, yakiwemo maeneo ya Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi Wembere na Songo Songo Magharibi, pamoja na mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia(LNG).

Agizo hilo lilitolewa wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa miaka 25 wa TPDC (2024/25 – 2049/50) tarehe 30.04.2025 Jijini Dodoma, ukiwa na lengo la kuongeza uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa soko la ndani na nje ya nchi.

Katika hotuba yake, Dkt. Biteko alisema mpango huo wa miaka 25 ni hatua muhimu katika kuhakikisha rasilimali za mafuta na




gesi zinachangia kikamilifu maendeleo ya Taifa. Alisisitiza kuwa sekta ndogo ya mafuta na gesi ina nafasi kubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi na hivyo TPDC inapaswa kuhakikisha usambazaji wa gesi unawafikia wananchi wengi kupitia teknolojia kama Mini-LNG na CNG.

Aidha, aliiagiza TPDC kujiimarisha kifedha kwa kubuni mifumo ya kibunifu ya utekelezaji wa miradi, kupunguza utegemezi kwa fedha za Serikali, na kuendelea na jitihada za kulipa mishahara kwa kutumia mapato ya ndani. Pia alisisitiza umuhimu wa shirika hilo kushirikiana na kampuni za kimataifa, wawekezaji binafsi na wadau wa maendeleo kwa kuzingatia misingi ya mazingira, jamii na utawala bora (ESG).

Katika hatua nyingine, Dkt. Biteko ameagiza TPDC kutoa kipaumbele kwa usambazaji wa gesi kwa matumizi ya kupikia ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni, hatua ambayo itasaidia kutunza mazingira na kupunguza hewa ukaa. Vilevile, alipongeza Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya TPDC kwa juhudi wanazofanya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha nishati katika ukanda huu.




# MKUU WA MKOA WA SINGIDA, MHE. HALIMA DENDEGO, ATEMBELEA BANDA LA GASCO KATIKA MAONESHO YA WIKI YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI

**Singida,**

Kampuni Tanzu ya GASCO (Gas Company) imeshiriki maadhimisho ya Wiki ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha masuala ya usalama na afya kazini. Maadhimisho hayo yalifanyika mkoani Singida.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Halima Dendego, alipata fursa ya kutembelea banda la GASCO kwenye viwanja vya maonesho yanayoratibiwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) na kujionea teknolojia mbalimbali na hatua zinazochukuliwa na GASCO katika kuhakikisha usalama wa wafanyakazi na mazingira ya kazi.
Akiwa katika banda hilo, Mhe. Dendego alielezwa kuhusu sera za usalama za kampuni, vifaa vya kisasa vinavyotumika kupunguza ajali, pamoja na mikakati endelevu ya kuhakikisha afya bora kwa wafanyakazi.

Aidha, Mhe. Dendego aliipongeza GASCO kwa jitihada madhubuti katika kuimarisha viwango vya usalama kazini huku akisisitiza kuwaTaasisi/ kampuni ziendelee kuimarisha usalama kazini ili kulinda rasilimali watu na kuongeza tija katika maeneo ya kazi.

“Usalama na afya mahali pa kazi ni wajibu wa kila mwajiri, GASCO wameonesha kwa vitendo uwekezaji sahihi katika sekta hii,” alisema Mhe. Dendego.

Wiki hii ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani mwaka huu inalenga kuhamasisha mazingira bora na salama ya kazi kwa kila mfanyakazi kupitia akili mnemba (AI) na teknolojia za kidigitali.

GASCO ni Kampuni tanzu ya TPDC inayojishughulisha na uendeshaji, matengenezo na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia.

# TPDC YADHAMINI NA KUSHIRIKI MKUTANO WA TEKNOLOJIA BARANI AFRIKA




**Mhandisi Koleta Selsi wa TPDC akitoa maelezo kuhusu nishati ya gesi asilia kwa washiriki wa mkutano waliotembelea banda la TPDC kwenye mkutano wa Teknolojia Barani Afrika uliofanyika Jijini Dar es salaam**

**Dar es Salaam,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeonesha kwa vitendo dhamira yake ya kukuza matumizi ya teknolojia bunifu katika sekta ya nishati kwa kushiriki na kudhamini Mkutano wa Teknolojia Afrika 2025 (Africa Technology Conference) uliofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia Mei 27 hadi 29, 2025.

Akizungumza wakati wa mkutano huo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) Mha. Charles Sangweni alisisitiza umuhimu wa kushiriki mikutano kwani inasaidia kuandaa vijana na wataalamu wa sekta

ya nishati kukabiliana na mabadiliko ya kiteknolojia yanayoendelea duniani.

“Kupitia mikutano hii, tunapata fursa ya kukutana na wenzetu kutoka sehemu mbalimbali za Dunia, ambapo tunabadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa wale waliopiga hatua za kiteknolojia na kusaidiana kuonyesha mwelekeo wa tasnia hii Duniani. Hii ni fursa muhimu pia ya kubadilishana uzoefu juu ya namna gani ya kuhusisha na kushirikisha wazawa (Local Content) ili kuhakikisha ushiriki wa wazawa na makampuni ya kitanzania unasimamiwa ipasavyo na kuendana na malengo ya Taifa,” alisema Mha. Sangweni.

Mkutano huo ni wa Kimataifa na umeandaliwa na Society of Petroleum Engineers (SPE) kwa ukanda wa Afrika ambapo umebeba kauli mbiu isemayo; “Kuelekea Mustakabali wa Kukuza Ubora wa Kiteknolojia kwa Maendeleo Endelevu ya Nishati Afrika,”

Aidha,Tanzania ni miongoni mwa nchi chache za Afrika ambazo zimeweza kuwa wenyeji wa mkutano huu, baada ya Nigeria, Ghana, Misri na Afrika Kusini ambapo tukio hili hufanyika mara moja kwa mwaka.



# TPDC YAKABIDHI VIFAA VYA OFISI KWA JESHI LA POLISI MTWARA

**Mtwara,**

Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilikabidhi vifaa vya ofisi (samani) vyenye thamani ya TZS Mil. 21 kwaajili ya Kituo cha Polisi cha Msimbati, kilichojengwa na TPDC chini ya maelekezo ya Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Tukio hilo lilifanyika katika ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Kanali Patrick Sawala, ambaye aliongoza hafla fupi ya makabidhiano.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara aliipongeza TPDC kwa kutekeleza maagizo ya Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ya ununuzi wa vifaa vya ofisi vya Kituo cha polisi Msimbati ambacho kimejengwa chini ya ufadhili wa TPDC.

"TPDC wamekuwa na utaratibu mzuri wa kurudisha kwa jamii faida wanayoipata kupitia miradi ya CSR. Kwa jeshi letu la Polisi walijenga kituo cha Polisi pale Msimbati na ilibaki samani za ofisi ili kianze kufanya kazi. Namshukuru Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa maelekezo yake na sasa yamefanyiwa kazi," alieleza Kanali Sawala.

Akizungumza wakati wa kukabidhi samani hizo, Afisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi wa TPDC, Ally Mluge kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo alisema Shirika hilo linaendelea kutekeleza wajibu wake wa kijamii kwa kushirikiana na Serikali na jamii katika maeneo linakotekeleza miradi yake. Ameongeza kuwa, utoaji wa vifaa hivyo ni ishara na dhamira ya Shirika katika kuimarisha uhusiano mwema na wadau mbalimbali, ikiwemo Jeshi la Polisi.




**Afisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi wa TPDC Bw. Ally Mluge, akikabidhi baadhi ya vifaa vya ofisi kwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Mhe. Kanali Patrick Sawala katika hafla iliyofanyika kwenye Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Mtwara**

Mluge aliongeza kuwa, vifaa vilivyokabidhiwa kwa Jeshi la Polisi ambavyo vinajumuisha kompyuta, printa, meza, viti, TV, king'amuzi na vifaa vingine muhimu vitasaidia kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa jeshi la Polisi.

"Tunaamini kwamba, vifaa hivi vitachangia katika kuongeza ufanisi wa kazi zao na kuimarisha hali ya utoaji huduma kwa Wananchi," alisema Mluge.

Katika hatua nyingine, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoani Mtwara, SACP Issa Sulemani ameishukuru TPDC kwa ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Msimbati pamoja na kuwanunulia vifaa vya ofisi vya kisasa. Vilevile amemshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha maboresho ya Jeshi la Polisi katika Nyanja zote.

# TPDC YATOA ELIMU KWA JAMII ZA WAVUVI KUHUSU MRADI WA UTAFUTAJI MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA KITALU CHA EYASI WEMBERE

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), katika kuendelea na utekeleza majukumu yake ya kisheria na kijamii, lilitekeleza zoezi la utoaji elimu kwa jamii za Wavuvi kuhusu mradi wa uchukuaji taarifa za mitetemo (seismic survey) kwaajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Wilaya za Meatu (Mkoa wa Simiyu) na Karatu (Mkoa wa Arusha).

Lengo la utoaji elimu hiyo ni kuhakikisha jamii inafahamu madhumuni ya uchukuaji wa taarifa za mitetemo, teknolojia inayotumika, athari zinazoweza kujitokeza, na hatua za tahadhari zinazochukuliwa ili kulinda mazingira na shughuli za kiuchumi kama vile uvuvi.



**Mhandisi Lucas Luhaga wa TPDC akitoa elimu juu ya mradi wa utafutaji wa mafuta na gesi kwa Wavuvi wa Kambi ya Mzungu iliyopo Kijiji cha Gidamilenda Wilaya ya Karatu**

Zoezi hilo lilifanyika tarehe 9-30 Aprili, 2025, likilenga kuhamasisha ushiriki na uelewa wa jamii hususan wale wanaofanya shughuli za uvuvi katika maeneo yanayopitiwa na mradi. Elimu hiyo ilitolewa kwa kambi kumi (10) za Wavuvi kutoka Kata ya Bukundi (Meatu) na Kata za Karatu (Karatu), ambapo jumuiya hizo ni miongoni mwa wadau muhimu katika maeneo ya utafiti.

Akizungumza wakati wa utoaji elimu Mkuu wa Wilaya ya Karatu Mhe. Dadi Horice Kolimba alisema, "ni hatua nzuri sana kwa Serikali kushirikisha na kutoa elimu kuhusu mradi kwa jamii mapema. TPDC iendelee na utaratibu huu hata wakati wa utekelezaji wa hatua nyingine ya mradi."

Naye, Mhandisi Lucas Luhaga, kutoka TPDC aliwaeleza Wavuvi kuwa teknolojia ya kisasa ya mitetemo inazingatia viwango vya kimataifa vya usalama wa mazingira na haiathiri viumbe hai wa majini. Pia alisisitiza kuwa zoezi hilo ni hatua ya awali tu ya utafutaji, hivyo jamii zitashirikishwa katika kila hatua ya mradi.
Hali kadhalika, Kiongozi wa Kambi ya Wavuvi katika Kijiji cha Bukundi Bw. Yohana Samson, aliishukuru TPDC kwa uwazi na juhudi za kuwashirikisha wananchi kupata uelewa wa mradi. Ushirikishwaji huu umechangia kupunguza hofu na kuongeza uelewa wa manufaa ya sekta ya mafuta na gesi kwa maendeleo ya taifa.

"Tunashukuru TPDC kwa elimu hii muhimu, imetusaidia kuelewa mchakato mzima wa utafutaji wa gesi na mafuta. Tumepata maarifa mapya ambayo yatatusaidia kushiriki kikamilifu bila hofu," alisema Yohana.

# TPDC YADHAMINI NA KUSHIRIKI MBIO ZA MARATHONI KWA LENGO LA KUELIMISHA UMMA MATUMIZI YA NISHATI SAFI



**Dar es salaam,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) liliungana na Wadau mbalimbali katika kushiriki mbio za marathoni zilizoandaliwa na Tanzania Business Women Association ( TABWA) kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini. Mbio hizo zilifanyika katika viwanja vya Green Ground, Oysterbay Jijini Dar es Salaam tarehe 17.05.2025 na zimehusisha wakimbiaji katika makundi mbalimbali za umbali wa kilomita 5, kilomita 10 na kilomita 21.

TPDC, kama Taasisi ya Umma yenye jukumu la kusimamia maendeleo ya rasilimali za mafuta na gesi asilia nchini, imeona umuhimu wa kutumia jukwaa hili kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu faida za kutumia nishati safi ya kupikia, hususan gesi asilia majumbani, kwa afya ya jamii na mazingira.

Katika kuhakikisha mafanikio ya tukio hilo muhimu, TPDC ilitoa udhamini wa shilingi milioni 20, ikiwa ni mchango wake katika kufanikisha maandalizi na uendeshaji wa mbio hizo. Udhamini huo ni sehemu ya dhamira ya Shirika katika kushirikiana na jamii kwenye shughuli za michezo.

Akizungumza kwa niaba ya TPDC, Mkurugenzi wa Biashara ya Gesi na Mafuta Mha.Emmanuel Gilbert alisema, “Ushiriki wetu katika mbio hizi ni sehemu ya jitihada za Shirika kuendelea kuhamasisha matumizi ya gesi asilia kama nishati safi ya kupikia, ambayo ni salama, rafiki kwa mazingira na yenye gharama nafuu kwa Wananchi.”

Mbali na kutoa udhamini, TPDC ilishiriki kikamilifu katika mbio hizo kupitia Wanachama wa klabu yake ya 'TPDC Runners'. Klabu hiyo imekuwa ikishiriki matukio mbalimbali ya michezo nchini kwa lengo la kulitangaza Shirika, kuimarisha afya za Wafanyakazi, pamoja na kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Wanariadha wa TPDC Runners walionesha ushindani na ari kubwa ya kushiriki, wakibeba ujumbe maalum juu ya umuhimu wa kuachana na matumizi ya kuni na mkaa, na badala yake kuchagua gesi asilia kama mbadala salama, nafuu na rafiki wa mazingira.

Kupitia ushiriki huo, TPDC inazidi kudhihirisha dhamira yake ya kuchangia katika ajenda ya taifa ya upatikanaji wa Nishati Safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034, sambamba na kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya madhara ya kiafya na kimazingira yatokanayo na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Katika hatua nyingine baadhi ya wanariadha kutoka TPDC walitoa maoni yao kuhusu umuhimu wa kutumia nishati safi.

“Mimi ni mtumiaji wa gesi asilia nyumbani. Gesi asilia ni salama kwa familia yangu na imenipunguzia gharama kubwa za kuni na mkaa,” alisema Bi. Eva Swilla wa TPDC Runners Club.

“Mbio hizi zimeleta uelewa kwa jamii. Tunaamini tukirudia mara kwa mara, tutaweza kubadilisha fikra za wengi kuhusu kupika kwa kutumia Nishati safi,” aliongeza Bi.Delian Kabwogi, mwanariadha kutoka TPDC.



Baadhi ya Wanachama wa TPDC Runners Club walioshiriki mbio za marathoni

# TPDC YATUNUKIWA TUZO YA UHIFADHI MAZINGIRA

**Dodoma,**

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilifanikiwa kutunukiwa Tuzo ya Uhifadhi wa Mazingira kwa mwaka 2025

Tuzo hiyo ilitolewa tarehe 08.06.2025 Jijini Dodoma na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango katika Kilele cha maadhimisho ya wiki ya Mazingira Duniani.

Aidha, Tuzo hiyo ililenga kutambua mchango wa TPDC katika uhifadhi wa mazingira kupitia usambazaji wa gesi asilia ya kupikia pamoja na matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri (CNG) kwa njia salama na rafiki kwa mazingira.

Hii ni sehemu ya juhudi za shirika hilo katika kukuza nishati safi na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa, ambayo huchangia uharibifu wa mazingira.

Pia, TPDC ilitambuliwa kwa kuendeleza matumizi ya gesi asilia kama mbadala wa nishati chafu, hatua inayosaidia kupunguza hewa ukaa na kulinda afya ya jamii.



**Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango akimkabidhi Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) CPA Mussa M. Makame tuzo ya kutambua mchango wa TPDC katika kuhifadhi na kutunza mazingira kupitia matumizi ya gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG)**

# MHE. KAPINGA AZINDUA KITUO MAMA CHA KUSHINDILIA GESI ASILIA KWENYE MAGARI




**Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga amezindua Kituo mama cha kushindilia gesi asilia kwenye magari, chenye uwezo wa kujaza gesi asilia kwenye magari 1200 kwa siku na kufanya kazi masaa 24.**

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Kituo hicho Mhe. Kapinga ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuhakikisha Kituo hicho kinatunzwa ili kiendelee kuwa mfano wa huduma bora za kiwango cha hali ya juu na kuzingatia masuala ya usalama na utunzaji wa mazingira.

Uzinduzi wa Kituo hicho ulifanyika tarehe 09.05.2025 katika eneo la Kituo hicho kilichopo Chuo Kikuu cha Dar es salaam Jijini Dar es salaam.

Mhe. Kapinga alisema Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kujaza magari nane (8) kwa wakati mmoja pamoja na kulisha vituo vingine vidogo na kuchochea ongezeko la vituo vingine vya CNG. Aidha, Kituo hicho pia kina uwezo wa kuwapatia nishati ya gesi asilia watumiaji mbalimbali kama vile Viwanda, Shule, Hoteli n.k.

''Kwa muda mrefu kiu kubwa na ndoto ya watumiaji wa vyombo vya moto vinavyotumia gesi asilia mkoani Dar es Salaam na nchini kwa ujumla kuona vituo vinaongezeka katika maeneo mbalimbali nchini. Hii ni kutokana na faida mbalimbali za matumizi ya gesi asilia katika vyombo vya moto,

ikiwemo punguzo kubwa la gharama ukilinganishwa na nishati nyingine kama mafuta,"alisema Kapinga.

Aidha, Kapinga alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono, mtazamo na maelekezo kwa Wizara ya Nishati ambayo yanaleta matokeo chanya, kielelezo mojawapo ni kukamilika kwa Kituo cha CNG.

''Namshukuru pia Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko kwa uongozi wake katika kuhakikisha upatikanaji na uendelezaji wa nishati unaimarika nchini kwa matumizi mbalimbali na siyo tu Nishati bali Nishati safi ambayo ni rafiki kwa mazingira na afya za wananchi wetu."

Naye, Mkurugenzi wa Biashara ya Mafuta na Gesi wa TPDC, Mha. Emmanuel Gilbert alisema kwamba Kituo hicho kina uwezo wa kuzalisha CNG kiasi cha futi za ujazo miloni 4.2 sawa na kilo 120,000 kwa siku. Kituo kina pampu nne zenye jumla ya nozeli nane na kukifanya kuwa na uwezo wa kuhudumia magari 8 kwa wakati mmoja na kwa siku kikitoa huduma hii kwa zaidi ya magari 1,200 kwa siku.







# HABARI KATIKA PICHA







**Mhandisi Felix Nanguka kutoka TPDC akipokea Cheti cha Shukrani kwa niaba ya TPDC kwa kufadhili Mkutano wa Kiteknolojia wa Afrika na usaidizi endelevu wa SPE (Society of Petroleum Engineers) kwa ujumla, mkutano huo ulifanyika katika hoteli ya Hyatt Regency Jijini Dar es salaam**



**Baadhi ya Watumishi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) wakishiriki Mkutano wa Kiteknolojia wa Afrika, mkutano huo ulifanyika katika hoteli ya Hyatt Regency Jijini Dar es salaam**






**Baadhi ya vifaa vya ofisi vilivyotolewa na TPDC kwa Jeshi la Polisi Mtwara kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Kata ya Msimbati, Mtwara**



**Baadhi ya Wageni mbalimbali waliohudhuria uzinduzi wa Mpango Mkakati wa TPDC wa miaka 25 uliozinduliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Doto Biteko tarehe 30.04.2025, Dodoma.**



**Maafisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wakitoa mafunzo kwa vitendo namna ya kukabiliana na majanga ya moto kwa Watumishi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Mikocheni, Dar es salaam**



**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC Mhe. Balozi Ombeni Sefue (wa kwanza kushoto mwa Rais) akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC Ndg. Mussa Makame (wa pili kushoto mwa Rais) mara baada ya kupokea tuzo ya moja ya Mashirika yaliyofanya vizuri katika kutoa gawio kwa Serikali toka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 10.06.2025 Ikulu, Jijini Dar es salaam**




## BODI YA WAHARIRI

**MHARIRI MKUU**

Marie Msellemu

**WAJUMBE**

Beatrice Peter
Oscar Mwakasege
Delian Kabwogi
Ally Mluge
Eugene Isaya
Francis Lupokela

**LIMETOLEWA NA:**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania
(TPDC)
PSSSF Kambarage Tower 8th Floor,
Jakaya Kikwete Road,
S.L.P 1191, Dodoma.
Telephone:+255262323519
Barua pepe: tpdcmd@tpdc.co.tz
Tovuti: www.tpdc.co.tz